JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Shule ya Sekondari Lukole**
**S.L.P 41**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule** 0763947164
**Makamu Mkuu wa Shule** 0629245446
**Mwalimu wa Nidhamu** 0655319002

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

**……………………………………………..**

**S.L.P……………………………………...**

**……………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUKOLE HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA MKOA WA KAGERA MWAKA ………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Lukole katika mwaka wa masomo wa ………… na atasoma tahasusi ya …………

**2.** Shule ya Sekondari Lukole ipo umbali wa Kilometa 22 kutoka mji mkuu wa Wilaya ya Ngara. Kutoka kituo cha mabasi Ngara mjini nauli ni sh 4000/= mpaka shuleni. Shule ipo eneo linaloitwa K9 ni karibu sana na barabara. Kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya Mwanza, Bukoba, Karagwe na Kahama washukie katika kituo cha mabasi cha K9 watakiona kibao cha shule, ni Mita 50 tu kutoka katika kituo hicho.

**3.** Muhula wa Masomo unaanza tarehe **…………**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………** Mwisho wa kuripoti ni tarehe**……………………...**

**4. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

### 4.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni shati mbili (02) kitamba aina ya harua mikono mirefu.

ii. Suruali mbili kwa wavulana Bluu Nyeusi (**Dark Blue)**. Kila suruali moja iwe na upana wa nchi 16 kwa chini inayogusa kiatu kwa urefu na iwe na mfuko mmoja nyuma, modo haziruhusiwi kabisa.

iii. Sketi mbili zenye rangi ya Bluu Nyeusi **(Dark Blue).** Kila sketi iwe ndefu mpaka chini kwenye kisigino.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba kwa wavulana na wasichana. Pia mvulana aje na mkanda wa ngozi mweusi.

v. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na tai ya shule inayopatikana shuleni

vi. Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

vii. Rangi ya hijabu iwe **Nyeupe** kwa wasichana wa kiisilamu.

viii. Sweta ya shule rangi ya bluu nyeusi

**NB**: **Sare zote hizo, zinapatikana karibu na maeneo ya shule.**

### 4.2 SARE BAADA YA MASOMO (SHAMBA DRESS).

i. Wavulana wanatakiwa kuwa na suruali mbili zenye rangi ya damu ya mzee zinapatikana shuleni. Kila suruali moja iwe na upana wa nchi 16 kwa chini inayogusa kiatu kwa urefu na iwe na mfuko mmoja nyuma, modo haziruhusiwi kabisa.

ii. Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee). Kila sketi iwe ndefu mpaka chini kwenye kisigino.

iii. Kila mwanafunzi atakuwa na T-shirt ya kushindia inayopatikana shuleni

iv. Sare ya michezo (Track suit kwa wasichana na wavulana) zinapatikana shulenizenye rangi ya bluu nyeusi **( dark blue**) na viatu vya michezo.

Kwa kuwa maeneo haya yana baridi sana, kila mwanafunzi atapaswa kuwa na sweta ya kuvaa baada ya masomo. Sweta inayoruhusiwa ni sweta nzito ya rangi **nyeusi** na si vinginevyo na isiwe na picha wala maandishi yoyote

**Nb. Sare zote zinapatikana karibu na maeneo ya shule**

### 4.2 Mahitaji muhimu mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

***VIFAA VYA USAFI***

i. Mifagio ya chelewa miwili. ii.

Fyekeo,

iii. Hard broom/soft bloom iv.

Reki/siko

v. Rubber squeezer

vi. Jembe na mpini

vii. Panga

**Angalizo: vitu vyote ni muhimu kwa ajili ya shughuli za mwanafunzi awapo shuleni na vinapatikana karibu na maeneo ya shule kwa bei ya kawaida.**

***VIFAA VYA KULALIA***

a. Godoro la 2 ½ x 6 linapatikana maeneo karibu na shuleni
b. Shuka 2 za rangi ya pinki
c. Blanket 1 ni **muhimu** kwa sababu eneo hili kuna baridi

***VIFAA VYA CHAKULA***

i. Sahani ii.

Bakuli iii.

Kijiko

iv. Kikombe cha ½ lita cha plastiki

**NB, Vifaa vyote hivi vinapatikana maeneo karibu na shule kwa kuepusha usumbufu kwa wazazi**

***VIFAA VYA DARASANI***

a. Counter book 8 (Quire Three) zinapatikana shuleni kwa bei ya sokoni.
b. Kalamu za kutosha,
c. Wanafunzi wa HGE, CBG na EGM waje na scientific calculator (**Non Programable Calculator)**. Pia, wanafunzi wote wanaosoma somo la Jiografia waje na **mathematical set**.
d. Wanafunzi wanaosoma tahasusi ya CBG waje na **Dissecting Kit**.

e. Wanafunzi wanunue Kamusi aina ya **Oxford Advanced Learners Dictionary** na kamusi sanifu ya Lugha ya Kiswahili kwa wanaosoma Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili

f. **Kila Muhula** mwanafunzi aje na rimu 1 ya karatasi aina ya **DOUBLE A KWA KILA MUHULA** kwa ajili ya majaribio na mitihani.

**NB, Vifaa vyote hivi vinapatikana maeneo karibu na shule**

***VIFAA VINGINEVYO***

i. Uje na vifaa vyako vya matumizi ya kila siku kama vile taulo, dawa za meno, mswaki, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta, ndoo, beseni, mto n.k. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyako. ii. **Nguo za kiraia ambazo si sare za shule, ambazo hazikutajwa katika fomu hii haziruhusiwi kuvaliwa shuleni**. iii. Kadi ya bima ya afya aina ya **NHIF** ni ya **MUHIMU** kwa kila mwanafunzi, hivyo ni muhimu kila mwanafunzi awe nayo.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**5. Michango mbalimbali**

**Angalizo: Jumla ya michango kwa Mwanafunzi ni shilingi 80,000/= (elfu themanini tu) kwa mchanganuo wa jedwali hapo juu.**

Fedha zote za michango ya shule zilipwe Benki kwenye Account ya shule; **Jina la Akaunti:** *LUKOLE SECONDARY SCHOOL CAPITATION GRANTS*

**Akaunti Namba:** ***32101200054*** **Tawi lolote** la **NMB au wakala wa NMB .** Tutapokea risiti ya Benki yenye jina la mwanafunzi. Aidha, kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonyesha aina ya malipo watakayolipiwa.

## 6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa; viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini/dhehebu wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa v. ujumla;
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu
vii. yeyote yule;
viii. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa
ix. mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
x. Kufuga ndevu;
xi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
xii. Uvutaji wa sigara;
xiii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xiv. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xv. Kusababisha mimba;
xvi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xvii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xviii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya
xix. shule;
xx. Kudharau Bendera ya Taifa;
xxi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

b. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**7. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iii. Picha Tatu (3) (passport size) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu vibandikwe kwenye fomu ya wazazi/walezi iliyoambatanishwa chini.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0763947164**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0629245446**
- **Mwandamizi Malezi: 0655319002**

THE HEADMISTRESS
LUKOLE SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 41
NGARA

……………………………………

*BONAVITANGANYAGWA*

*MKUUWASHULE*

## FOMUHIIIJAZWENAIREJESHWESHULENI

Mimi (Jina la Mwanafunzi) ………………………………………………… naahidi kuwa mtiifu wa sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa shuleni kwa mfano: kumiki simu shule, kushiki kwenye migomo, fujo, makosa ya jinai n.k.

Sahihi …………………………………… (Mwanafunzi) Tarehe …………………………

Mimi (Jina la Mzazi/mlezi) ……..…………..……………………………………………. Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………… nakiri kusoma maelekezo na masharti yote ya shule, nakubaliana na sheria, kanuni, taratibu, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi ………………… (Mzazi/mlezi) Simu ……………… Tarehe …………………...

Namba za simu na picha za wazazi/walezi

(i) Jina ………………………………… No. Simu …………………. Uhusiano ……………

PICHA

(ii) Jina ………………………………… No. Simu …………………. Uhusiano ……………

PICHA

(iii) Jina………………………………...No. Simu……………………...Uhusiano…………..........................

PICHA

## FOMUHIIIJAZWENAIREJESHWESHULENI

Mimi mzazi/mlezi wa ………………………………………………… nakiri kusoma na kuelewa masharti yote yaliyomo ndani ya fomu ya kujiunga na shule ya sekondari Lukole. Naahidi kutekeleza jukumu langu la uzazi/ulezi kwa mwanagu.

Ninakiri pia kuzungumza na kumwelekeza namna bora ya kuishi akiwa shuleni, hivyo kutojihushisha na makundi ovu ya wanafunzi wenzake na kupelekea uvunjifu wa amani wa aina yoyote ikiwa ni Pamoja na mwanangu kutokumiliki na kutumia simu kinyume na utaratibu uliowekwa na shule katika kipindi chote cha masomo yake akiwa shule ya sekondari Lukole. Naahidi pia kuendelea kushirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha tunamlea mwanetu katika maadili yaliyomema.

Jina…………………………………… sahihi ………… Tarehe ……………… namba ya simu…………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

**DATE…………………**

**STUDENT'S NAME ………………………………….………………….. (NAME IN FULL)**

THE MEDICAL OFFICER:

……………………………………….

………………………………………..

………………………………………..

I have examined the abovenamed student and consider him/her physically and mentally fit for his/her studies. The examination has included the following categories:

a) Eye – sight …………………………………………………….…………...
b) Hearing ……………………………………………………………….….……
c) Limbs …………………………………………………………….…………
d) Venereal diseases ……………………………………………….....…...
e) Epilepsy ……………………………………………………….…………
f) Leprosy ………………………………………………………………....….
g) Neuroses ……………………………………………………………….
h) Other serious Diseases …………………………………………………….
i) Pregnancy ………………………………………………………………

Date ……………………………… Signature …………………………

Station …………………………… Designation ………………………